# NENO KAFANYIKA MWILI

TAMKO LA LIGONIER

KUHUSU KRISTOLOJIA

# NENO KAFANYIKA MWILI

TAMKO LA LIGONIER KUHUSU KRISTOLOJIA

Ligonier Ministries

Neno Kafanyika Mwili: Tamko la Ligonier Kuhusu Kristolojia
Hakimiliki © 2016 na Ligonier Ministries

Toleo la Pili
Limechapishwa na Ligonier Ministries
421 Ligonier Court, Sanford, FL 32771
Ligonier.org | ChristologyStatement.com
Nukuu zote za Maandiko zimetolewa kwenye The Holy Bible, English Standard Version,
hakimiliki © 2001 na Crossway Bibles, kitengo cha Good News Publishers.
Kutumika kwa idhini. Haki zote zimehifadhiwa.

Je, Yesu Kristo ni nani? Karibu kila mtu mzima anayo maoni fulani kumhusu Yesu. Maoni haya huenda yakawa ya juu juu, yasiyo na ufahamu, au hata ya kizushi kabisa. Ukweli kumhusu Yesu, wala sio maoni tu, ni muhimu . . . umuhimu wa milele.

Wale wanaochukua jina Mkristo wanakiri kumfuata Kristo kama wanafunzi wake. Wanashika Kristolojia—mafundisho—ambalo linaakisi mtazamo wao wa Kristo. Kristolojia huenda ikaelezwa kwa njia isiyo wazi au iliyo wazi. Inaweza kuwakilisha kina cha ufunuo wa kibiblia na mawazo ya kihistoria ya Kikristo kuhusu Maandiko, ama inaweza ikawa mpya na isiyoungana na Neno la Mungu. Lakini hakuna akiriye kuwa Mkristo ambaye hana Kristolojia.

Kwa kuwa kumfuata Kristo ni jambo la kimsingi katika Ukristo, kanisa limefanya kazi kwa karne nyingi kumtangaza Kristo wa historia na Maandiko, wala si Kristo wa kujidhania kwetu. Katika matamko ya kihistoria ya imani kama vile Kanuni ya Imani Ya Nikea, Fasili Ya Kalsedonia, Katekisimu Ya Haidelbagi, na Ungamo la Westminsta, Wakristo wameeleza mafundisho ya kibiblia kumhusu Kristo.

Leo hii, matamko haya mara nyingi hupuuzwa na kueleweka vibaya, Leo hii, matamko haya mara nyingi hupuuzwa au kueleweka vibaya, jambo linalochangia mkanganyiko ulioenea kuhusu nafsi na kazi ya Kristo.. Kwa ajili ya utukufu wa Kristo na kujengeka kwa watu Wake, Tamko la Ligonier kuhusu Kristolojia linalenga kuwasilisha Kristolojia ya kihistoria, sahihi, na ya kibiblia ya Kanisa la Kikristo kwa namna iliyo rahisi kuungamwa, yenye manufaa kwa kufundisha imani ya Kanisa idumuyo, na inayoweza kutumika kama ungamo la pamoja ambalo waumini kutoka makanisa mbalimbali wanaweza kulikubali na kushirikiana katika kazi ya umisheni. Tamko hili halichukui nafasi ya kanuni za imani na maungamo ya kihistoria ya kanisa ila ni kijalizo kinachoelezea ujumla wa mafundisho yao kuhusu Kristo ni nani na kile alichokifanya. Kristo na akalitumie tamko hili kwa ajili ya ufalme wake.

Katika jina la Mwana wa Mungu aliyefanyika mwili, Nabii wetu, Kuhani, na Mfalme.

R.C. SPROUL

MAJIRA YA KUCHIPUA 2016

Tunaungama siri na ajabu
Ya Mungu aliyefanyika mwili
na kufurahia wokovu wetu mkuu
kupitia Yesu Kristo Bwana wetu.

Pamoja na Baba na Roho Mtakatifu,
Mwana aliviumba vitu vyote,
huvihimili vitu vyote,
na huvifanya vitu vyote kuwa vipya.
Mungu kweli,
alifanyika mwanadamu kweli,
asili mbili katika nafsi moja.

Alizaliwa na Bikira Maria
na akaishi miongoni mwetu.
Alisulubiwa, akafa, na kuzikwa.
Alifufuka siku ya tatu,
akapaa mbinguni,
na atakuja tena
katika utukufu na hukumu.

Kwa ajili yetu,

Aliishika Sheria,

akafanya upatanisho kwa ajili ya dhambi,

akairidhisha ghadhabu ya Mungu.

Alichukua matambara yetu machafu,

Akatupatia

Joho lake la haki.

Yeye ni Nabii wetu, Kuhani, na Mfalme,

akilijenga kanisa lake,

akiomba kwa ajili yetu,

na akitawala juu ya vyote.

Yesu Kristo ni Bwana;

Tunalihimidi Jina lake takatifu milele.

Amina.

# Uthibitisho Na Makanusho

*Pamoja na Ithibati za Maandiko*

*Kipengele 1*

Tunasadiki kwamba Yesu ndiye mfanyika mwili katika historia ya Mwana wa milele wa Mungu, nafsi ya pili ya Utatu Mtakatifu. Yeye ni Kristo, Masihi[1] wa Mungu aliyeahidiwa.

Tunakanusha, kwamba Kristo ni mwanadamu tu au kwamba alikuwa kiumbe wa kubuniwa na kanisa la Kristo pale mwanzoni.

*Kipengele 2*

Tunasadiki kwamba katika umoja wa Uungu, Mwana aliyezaliwa tangu milele ana asili moja, ni sawa kwa mamlaka, na wa umilele na Baba pamoja na Roho Mtakatifu[2]..

Tunakanusha, kwamba Mwana yupo tu kama Mungu (homoiousios) au kwamba aliasilishwa tu na Baba kama Mwanawe. Tunakanusha kutiishwa milele kwa Mwana kwake Baba katika Utatu wa kiontolojia.

*Kipengele 3*

Tunasadiki, pamoja Imani za Nikea na Kalsedonia, kwamba Yesu Kristo ni Mungu kweli na ni mwanadamu kweli, asili mbili zilizoungana katika nafsi moja milele[3].

Tunakanusha, kwamba Mwana aliumbwa. Tunakanusha kwamba kumewahi kuwa na wakati ambapo Mwana hakuwa Mungu. Tunakanusha kwamba mwili wa kibinadamu na nafsi ya Yesu Kristo ilikuwepo kabla ya Mwana kufanyika mwili katika historia.

---

1 Hapo mwanzo alikuwako Neno, naye Neno alikuwako pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu . . . Naye Neno akafanyika mwili na akakaa miongoni mwetu, nasi tumeuona utukufu wake, utukufu kama wa Mwana wa pekee atokaye kwa Baba, aliyejaa neema na kweli (Yohana 1:1, 14). Tazama pia Zab. 110:1; Mt. 3:17; 8:29: 16:16; Marko 1:1, 11; 15:39; Luka 22:70; Yohana 4:25-26; Matendo 5:42; 9:22; Gal. 4:4; Flp. 2:6; Kol. 2:9; Ebr. 5:7; 1 Yoh. 5:20

2 Basi nendeni mkayafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza katika jina la Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu (Mt. 28:19). Tazama pia Yohana 1:18; 3:16-18; 10:30; 20:28; 2 Kor. 13:14; Efe. 2:18.

3 Maana katika yeye unakaa utimilifu wote wa Uungu, kwa jinsi ya kimwili (Kol. 2:9). Tazama pia Luka 1:35; Yohana 10:30; Rum. 9:5 1 Tim. 3:16; 1 Pet. 3:18.

*Kipengele 4* Tunasadiki ule muungano wa asili, kwamba zile asili mbili za Yesu Kristo zimeungana katika nafsi yake moja pasipo kuchangamana, kukanganyika, kugawanywa, wala kutengana[4].

Tunakanusha kwamba kutofautisha baina ya asili hizi mbili ni kuzitenganisha.

*Kipengele 5* Tunasadiki kwamba katika kufanyika mwili kwa Yesu Kristo, asili zake za kiungu na kibinadamu zinadumisha sifa zake zenyewe. Tunakiri kwamba sifa za asili zote mbili ni za ile nafsi moja Yesu Kristo[5].

Tunakanusha, kwamba asili ya kibinadamu ya Yesu Kristo inazo sifa za kiungu au inaweza kuchukua asili ya kiungu. Tunakanusha, kwamba asili ya kiungu huwasilisha sifa za kiungu kwa ile asili ya kibinadamu. Tunakanusha, kwamba Mwana aliweka kando au alisalimisha sifa iwayo yoyote ya kiungu katika kufanyika mwili kwake.

---

4 Simoni Petro akajibu, "Wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai." Na Yesu akamjibu, "Umebarikiwa wewe Simoni Bar-Yona! Maana mwili na damu havikukufunulia hili, bali Baba yangu aliye mbinguni" (Mt. 16:16-17). Tazama pia Luka 1:35; Yohana 1:1-3; 8:58; 17:5; Mdo. 20:28; Rum. 1:3; 9:5; 2 Kor. 8:9; Kol. 2:9; 1 Tim. 3:16; 1 Pet. 3:18; Ufu. 1:8, 17; 22:13

5 Muwe na akili hii miongoni mwenu, ambayo ni yenu katika Kristo Yesu, ambaye, ingawa alikuwa katika namna ya Mungu hakuhesabu kuwa sawa na Mungu kama kitu cha kushikamana nacho ila alijimimina kwa kuchukua namna ya mtumishi, akizaliwa katika mfano wa wanadamu (Flp. 2:5-7). Tazama pia Mt. 9:10; 16:16; 19:28; Yohana 1:1; 11:27, 35; 20:28; Rum. 1:3-4; 9:5; Efe. 1:20-22; Kol. 1:16-17; 2:9-10; 1 Tim. 3:16; Ebr. 1:3, 8-9; 1 Pet. 3:18; 2 Pet. 1:1.

*Kipengele 6* Tunasadiki kwamba Yesu Kristo ndiye mfano unaoonekana wa Mungu, kwamba yeye ndiye kigezo cha ubinadamu wa kweli, na kwamba katika kukombolewa kwetu hatimaye tutafanywa kuwa sawa na mfano wake[6].

Tunakanusha, kwamba Yesu Kristo alikuwa chochote kile ila mwanadamu wa kweli, kwamba alionekana tu kuwa kama mwanadamu, au kwamba hakuwa na roho ya kimantiki ya kibinadamu. Tunakanusha, kwamba katika ule muungano wa asili Mwana alijichukulia nafsi ya kibinadamu badala ya asili ya kibinadamu.

*Kipengele 7* Tunasadiki kwamba akiwa mwanadamu kweli, Yesu Kristo katika hali yake ya kufedheheshwa alikuwa na mipaka ya kawaida na mapungufu ya kawaida ya asili ya kibinadamu. Tunasadiki kwamba alifanywa kuwa kama sisi katika kila jambo, ila alikuwa hana dhambi.[7]

Tunakanusha, kwamba Yesu Kristo alitenda dhambi. Tunakanusha kwamba Yesu Kristo hakupitia kuteseka, kujaribiwa, au magumu. Tunakanusha kwamba dhambi huishi katika ubinadamu wa kweli au kwamba kutokuwa na dhambi kwa Yesu Kristo hakuambatani na yeye kuwa mwanadamu wa kweli.

---

6 Yeye ndiye mfano wa Mungu asiyeonekana, mzaliwa wa kwanza wa uumbaji wote. Kwa kuwa kwa yeye vitu vyote viliumbwa, mbinguni na duniani, vinavyoonekana na visivyoonekana, viwe viti vya enzi au mamlaka au wakuu au watawala–vitu vyote viliumbwa kumpitia yeye na kwa ajili yake (Kol. 1:15-16). Tazama pia Rum. 8:29; 2 Kor. 4:4–6; Efe. 4:20-24; Ebr. 1:3-4.

7 Kwa hiyo ilimpasa kufanywa kama ndugu zake katika kila njia, ili kwamba apate kuwa kuhani mkuu mwenye rehema na mwaminifu katika huduma ya Mungu, kufanya upatanisho kwa ajili ya dhambi za watu. Kwa kuwa kwa sababu yeye mwenyewe ameteseka alipojaribiwa, anaweza kuwasaidia wale wanaojribiwa (Ebr. 2:17-18). Tazama pia Mik. 5:2; Luka 2:52; Rum. 8:3; Gal. 4:4; Flp. 2:5-8; Ebr. 4:15

*Kipengele 8* Tunasadiki kwamba Yesu wa kihistoria, kwa uweza wa Roho Mtakatifu, alichukuliwa mimba kimuujiza, na akazaliwa na Bikira Maria. Tunasadiki pamoja na Kanuni ya Imani ya Kalsedonia kwamba anaitwa kwa usahihi mama wa Mungu (theotokos) kwa maana mtoto aliyemzaa ndiye Mwana wa Mungu aliyefanyika mwili, nafsi ya pili katika Utatu Mtakatifu[8].

Tunakanusha kwamba Yesu Kristo aliipokea asili yake ya kiungu kutoka kwa Maria au kwamba kutokuwa na dhambi kwake kulitokana na Maria.

*Kipengele 9* Tunasadiki kwamba Yesu Kristo ndiye Adamu wa mwisho aliyefaulu katika kazi aliyoitiwa katika kila jambo ambapo Adamu wa kwanza alishindwa, na kwamba Yesu Kristo ndiye kichwa cha watu wake, ule mwili wa Kristo[9].

Tunakanusha, kwamba Yesu Kristo alijichukulia asili ya kibinadamu iliyoanguka au kwamba alirithi dhambi ya asili.

---

8 Katika mwezi wa sita malaika Gabrieli alitumwa kutoka kwa Mungu kwenda mji wa Galilaya uitwao Nazareti, kwa bikiria aliyeposwa kwa mtu ambaye jina lake lilikuwa Yusufu, wa nyumba ya Daudi. Na jina la bikira lilikuwa Maria (Luka 1:26-27). Tazama pia Mt. 1:23; 2:11; Luka 1:31, 35, 43; Rum. 1:3; Gal. 4:4.

9 Kwa hiyo, kama vile dhambi ilivyoingia ulimwenguni kwa mtu mmoja, na mauti kwa dhambi; na hivyo mauti ikawafikia wanadamu wote kwa sababu wote walifanya dhambi - kwa maana dhambi kweli ilikuwamo duniani kabla ya sheria kutolewa, lakini dhambi haihesabiwi isipokuwapo sheria; ila mauti ilitawala tangu Adamu mpaka Musa, hata juu ya wale ambao kutenda dhambi kwao hakukuwa kama kosa la Adamu aliye mfano wa kutimizwa wake yeye atakayekuja. Lakini ile karama ya bure sio kama lile kosa; kwa maana ikiwa kwa kosa la mtu mmoja wengi walikufa, zaidi sana neema ya Mungu, na ile karama ya bure kwa neema yake yule mtu mmoja Yesu Kristo vimezidi kwa ajili ya wale wengi. Nayo karama ya bure sio kama tokeo la dhambi ya yule mtu mmoja. Kwa kuwa hukumu iliyofuata kosa moja ilileta adhabu, lakini karama ya bure iliyofuata makosa mengi ilileta kuhesabiwa haki. Kwa maana ikiwa kwa sababu ya kosa la mtu mmoja mauti ilitawala kwa huyo mtu mmoja, zaidi sana wao wapokeao wingi wa neema, na karama ya bure ya haki, watatawala katika uzima kwa yule mtu mmoja, Yesu Kristo. Kwa hiyo, kama vile kosa lilipeleka kwenye adhabu kwa watu wote, kadhalika tendo moja la haki linapeleka kwenye kuhesabiwa haki na uzima kwa watu wote. Kwa kuwa kama kwa kuasi kwa yule mtu mmoja wale wengi walifanywa wenye dhambi, kadhalika kwa kutii kwake yule mtu mmoja wale wengi watafanyika wenye haki. Sasa sheria iliingia ili kuliongeza kosa; ila pale dhambi ilipoongezeka, neema ilikuwa nyingi zaidi; ili kwamba, kama vile dhambi ilivyotawala katika mauti, vivyo hivyo neema itawale kwa njia ya haki hadi uzima wa milele kwa Yesu Kristo Bwana wetu (Rum. 5:12-21. Tazama pia 1 Kor. 15:22, 45-49; Efe. 2:14-16; 5:23; Kol. 1:18.

*Kipengele 10* Tunasadiki ule utiifu wa kutenda na kutendewa wa Yesu Kristo, kwamba katika maisha yake makamilifu alitimiza kitimilifu madai ya haki ya sheria kwa niaba yetu, na kwamba aliichukua adhabu ya dhambi yetu kwa kifo chake msalabani[10].

Tunakanusha, kwamba Yesu Kristo katika hatua yoyote ile alikosa kutii au kuitimiza sheria ya Mungu. Tunakanusha kwamba alibatilisha sheria ya kimaadili.

*Kipenegel 11* Tunasadiki kwamba pale msalabani, Yesu Kristo alijitoa kama upatanisho mbadala wa adhabu kwa ajili ya dhambi za watu wake, akiondoa ghadhabu ya Mungu na kuridhisha haki ya Mungu, na kwamba alikuwa mshindi juu ya dhambi, mauti, na Shetani[11].

Tunakanusha, kwamba kifo cha Yesu kilikuwa malipo ya fidia kwa Shetani. Tunakanusha, kwamba kifo cha Yesu kilikuwa mfano tu, ushindi tu juu ya Shetani, au onyesho tu la utawala wa kimaadili wa Mungu.

---

10 Kwa kuwa kama kwa kuasi kwa yule mtu mmoja wale wengi walifanywa wenye dhambi, kadhalika kwa kutii kwake yule mtu mmoja wale wengi watafanyika wenye haki (Rum. 5:19). Tazama pia Mt. 3:15; Yohana 8:29; 2 Kor. 5:21; Flp. 2:8; Ebr. 5:8

11 Ambaye Mungu alimweka awe ondoleo la ghadhabu kwa njia ya imani katika damu yake, la kupokewa kwa imani. Hili lilikuwa kwa ajili ya kuonyeshe haki ya Mungu kwa sababu katika ustahimili wa kiungu alikuwa ameziachilia dhambi za zamani. Hili lilikuwa kwa ajili ya kuonyesha haki yake wakati huu, ili awe mwenye haki na mwenye kumhesabia haki yeye amwaminiye Yesu (Rum. 3:25-26). Tazama pia Isa. 53; Rum. 5:6, 8, 15; 6:10; 7:4; 8:34; 14:9, 15; 1 Kor. 15:3; Efe. 5:2; 1 The. 5:10; 2 Tim. 2:11; Ebr. 2:14, 17; 9:14-15; 10:14; 1 Pet. 2:24; 3:18; 1 Yohana 2:2; 3:8; 4:10.

*Kipengele 12* Tunasadiki fundisho la kuhesabiwa kuwili, kwamba dhambi yetu inahesabiwa kwake Yesu Kristo na haki yake inahesabiwa kwetu sisi kwa imani[12].

Tunakanusha, kwamba dhambi inakosa kutiliwa maanani pasipo hukumu. Tunakanusha kwamba utiifu wa kutenda wa Yesu Kristo hauhesabiwi kwetu.

*Kipengele 13* Tunasadiki kwamba siku ya tatu Yesu Kristo alifufuka kutoka kwa wafu na kwamba alionekana katika mwili na watu wengi[13].

Tunakanusha, kwamba Yesu Kristo alionekana tu kama aliyekufa, au kwamba ni roho yake tu iliyonusurika, au kwamba ufufuo wake ulifanyika tu mioyoni mwa wafuasi wake.

---

12 Kwa ajili yetu alimfanya yeye asiyejua dhambi kuwa dhambi, ili sisi tupate kuwa haki ya Mungu katika yeye (2 Kor. 5:21). Tazama pia Mt. 5:20; Rum. 3:21-22; 4:11; 5:18; 1 Kor. 1:30; 2 Kor. 9:9; Efe. 6:14; Flp. 1:11; 3:9; Ebr. 12:23.

13 Kwa maana niliwaletea ninyi kama vilivyo vya umuhimu mkuu vile ambavyo mimi pia nilivipokea: kwamba Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zetu kulingana na Maandiko, kwamba alizikwa, kwamba alifufuliwa siku ya tatu kulingana na Maandiko, na kwamba alitokea kwa Kefa, kisha kwa wale Kumi na Wawili (1 Kor. 15:3-5). Tazama pia Isa. 53; Mt. 16:21; 26:32; 28:1-10; Yohana 21:14; Mdo. 1:9-11; 2:25, 32; 3:15, 26: 4:10; 5:30; 10:40; Rum. 4:24-25; 6:9-10; Efe. 4:8-10.

*Kipengele 14* Tunasadiki kwamba katika hali yake ya kuinuliwa Yesu Kristo ndiye limbuko la ufufuo, kwamba ameshinda dhambi pamoja na mauti, na kwamba katika muungano naye sisi pia tutafufuliwa[14].

Tunakanusha, kwamba mwili uliotukuka na uliofufuliwa wa Yesu Kristo ulikuwa mwili tofauti kabisa na ule uliolazwa pale kaburini katika bustani. Tunakanusha, kwamba ufufuo wetu ni wa roho zetu tu mbali na miili yetu.

*Kipengele 15* Tunasadiki kwamba Yesu Kristo alipaa hadi kwenye kiti chake cha enzi mbinguni katika mkono wa kuume wa Mungu Baba, kwamba anatawala kwa wakati huu kama mfalme, na kwamba atarudi kwa njia ya kuonekana katika uweza na utukufu[15].

Tunakanusha, kwamba Yesu Kristo alikosea kuhusu habari ya wakati wa kurudi kwake.

---

14 Lakini kwa kweli Kristo amefufuliwa kutoka kwa wafu, malimbuko ya wale waliokwisha kulala . . .”Ewe mauti, uko wapi ushindi wako? Ewe mauti uko wapi uchungu wako?“ (1 Kor. 15:20, 55). Tazama pia Rum. 5:10; 6:4, 8, 11: 10:9; 1 Kor. 15:23; 2 Kor. 1:9; 4:10-11; Efe. 2:6; Kol. 2:12; 2 The. 2:13; Ebr. 2:9, 14; 1 Yohana 3:14; Ufu. 14:4; 20:14.

15 Basi walipokuja pamoja wakamuuliza, ”Bwana, utaurejesha ufalme kwa Israeli kwa wakati huu? Akawaambia, ”Haiwahusu ninyi kujua nyakati wala majira ambayo Baba ameyaweka kwa mamlaka yake. Ila mtapokea uweza Roho Mtakatifu atakapokuja juu yenu, nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu, na katika Yudea yote na Samaria, na hata miisho ya dunia.“ Na aliposema mambo hayo, walipokuwa wakiangalia, aliinuliwa juu, nalo wingu likamchukua kutoka machoni pao. Na walipokuwa wakiangalia juu mbinguni akienda zake, tazama, watu wawili walisimama kando yao wakiwa wamevaa majoho meupe nao wakasema, ”Watu wa Galilaya, mbona mnasimama mkiangalia juu mbinguni? Huyu Yesu aliyechukuliwa kutoka kwenu kwenda juu mbinguni atarudi kwa njia iyo hiyo mlivyomwona akienda zake mbinguni” (Mdo. 1:6-11). Tazama pia Luka 24:50-53; Mdo. 1:22; 2:33-35; Efe. 4:8-10; 1 Tim. 3:16

*Kipengele 16* Tunasadiki kwamba Yesu Kristo alimimina Roho wake siku ya Pentekoste na kwamba katika wakati wake huu anatawala juu ya vyote, akiwaombea watu wake, akilijenga kanisa lake, ambamo yeye ndiye kichwa pekee[16].

Tunakanusha, kwamba Kristo alimteua askofu wa Roma kuwa mwakilishi wake, au kwamba mtu yeyote mwingine mbali na Yesu Kristo anaweza kuwa kichwa cha kanisa.

*Kipengele 17* Tunasadiki kwamba Yesu Kristo atakuja tena katika utukufu kuwahukumu watu wote na kwamba hatimaye atawashinda maadui zake wote, atayaangamiza mauti, na kutuongoza katika mbingu mpya na dunia mpya ambamo atatawala katika haki[17].

Tunakanusha, kwamba kurudi kwa mara ya mwisho kwa Yesu Kristo kulifanyika mnamo 70 B.K. na kwamba ujio wake na matukio yanayoambatana nayo yanapaswa kuchukuliwa kama ya kiishara tu.

*Kipengele 18* Tunasadiki kwamba wale wanaoliamini jina la Bwana Yesu Kristo watakaribishwa katika ufalme wake wa milele, lakini wale wasiomwamini watateseka adhabu ya milele jehanamu wakiwa katika fahamu zao.[18]

Tunakanusha, kwamba kila mtu ataokolewa. Tunakanusha kwamba wale watakaokufa bila imani katika Yesu Kristo wataangamizwa hata wasikuwepo tena.

---

16 Naye akaviweka vitu vyote chini ya miguu yake na akamtoa kama kichwa juu ya vitu vyote kwa kanisa (Efe. 1:22). Tazama pia Mdo. 2:33; 1 Kor. 11:3-5; Efe. 4:15; 5:23; Kol. 1:18.

17 Naye alituamuru tuwahubirie watu na kushuhudia kwamba yeye ndiye aliyeteuliwa na Mungu kuwahukumu walio hai na wafu (Mdo. 10:42). Tazama pia Yohana 12:48; 14:3; Mdo. 7:7; 17:31; 2 Tim. 4:1, 8.

18 Mwana wa Adamu atawatuma malaika wake na watakusanya kutoka ufalme wake sababu zote za dhambi na wavunja sheria wote na kuwatupa katika tanuri iwakayo moto. Katika mahali pale kutakuwepo kulia na kusaga meno. Kisha wenye haki watang'aa kama jua katika ufalme wa Baba yao. Aliye na masikio na asikie (Mt. 13:41-43). Tazama pia Isa. 25:6-9; 65:17-25; 66:21-23; Dan. 7:13-14; Mt. 5:29-30; 18:8-9; Marko 9:42-49; Luka 1:33; 12:5; Yohana 18:36; Kol. 1:13-14; 2 The. 1:5-10; 2 Tim. 4:1, 18; Ebr. 12:28; 2 Pet. 1:11; 2:4; Ufu. 20:15.

*Kipengele 19*

Tunasadiki kwamba wote waliochaguliwa katika Yesu Kristo kabla ya kuwekwa kwa misingi ya ulimwengu na walioungamanishwa naye kwa njia ya imani wanafurahia ushirika pamoja naye na pia wao kwa wao. Tunasadiki kwamba katika Yesu Kristo tunafurahia kila baraka ya kiroho, ikiwemo kuhesabiwa haki, kuasiliwa, kutakaswa, na kutukuzwa[19].

Tunakanusha, kwamba Kristo na kazi yake iokoayo huweza kutenganishwa. Tunakanusha, kwamba tunaweza kushiriki katika kazi iokayo ya Yesu Kristo mbali na Yesu Kristo mwenyewe. Tunakanusha, kwamba tunaweza kuwa tumeungamanishwa na Yesu Kristo na huku tusiwe tumeungamanishwa na mwili wake, kanisa.

*Kipengele 20*

Tunasadiki fundisho la kuhesabiwa haki kwa imani pekee, kwamba Mungu hututangaza kuwa wenye haki kwa tendo la neema yake pekee kwa njia ya imani yetu pekee katika nafsi na kazi ya Yesu Kristo pekee, mbali na kustahili kwetu au matendo. Tunasadiki kwamba kulikana fundisho la kuhesabiwa haki kwa imani pekee ni kuikana Injili.[20]

Tunakanusha kwamba tunahesabiwa haki kwa msingi wa kujazwa kokote kule kwa neema ndani mwetu. Tunakanusha kwamba tunahesabiwa haki pale tu tunapokuwa wenye haki kiasili. Tunakanusha kwamba kuhesabiwa haki huku, sasa au wakati wowote ule kutawahi kuwa kwa misingi ya uaminifu wetu.

---

19 Maana katika Roho tulibatizwa sote katika mwili mmoja ---Wayahudi au Wayunani, watumwa au huru — na sote tulinyweshwa Roho mmoja (1 Kor. 12:13). Tazama pia Yohana 14:20; 15:4-6; Rum. 6:1-11; 8:1-2; 12:3-5; 1 Kor. 1:30-31; 6:15-20; 10:16-17:12:27: 2 Kor. 5:17-21; Gal. 3:25-29; Efe. 1:3-10, 22-23; 2:1-6; 3:6; 4:15-16; 5:23, 30; Kol. 1:18; 2:18-19.

20 Hivyo basi kwa kuwa tumehesbiwa haki kwa njia ya imani tunayo amani na Mungu kwa Bwana wetu Yesu Kristo (Rum. 5:1). Tazama pia Luka 18:14; Rum. 3:24; 4:5; 5:10; 8:30:10:4; 1 Kor. 6:11; 2 Kor. 5:19, 21; Gal. 2:16-17; 3:11, 24; Efe. 1:7; Tito 3:5, 7.

*Kipengele 21* Tunasadiki fundisho la utakaso, kwamba Mungu, kwa uweza wa Roho Mtakatifu, kwa msingi wa kazi ya Yesu Kristo, hutukomboa kutoka kwa nguvu zinazotawala za dhambi, hututakasa na hutufanya watakatifu kwa kutafanya zaidi na zaidi tufanane na mfano wa Mwanawe. Tunsadiki kwamba utakaso ni kazi ya neema ya Mungu na umeshikamana kwa njia isiyochangukana na kuhesabiwa haki, japo ni tofauti na kuhesabiwa haki. Tunasadiki kwamba katika kazi hii ya kiungu ya utakaso sio kwamba tunatendewa tu, bali tunawajibika kujitahidi kutumia zile njia zilizowekwa za neema katika juhudi zetu endelevu ili kuifia dhambi na kuishi katika utii kwa Bwana[21].

Tunakanusha kwamba mtu anahesabiwa haki pasipo yeye mara moja kuzaa matunda ya muungano wake pamoja na Yesu Kristo katika utakaso. Tunakanusha kwamba matendo yetu mema, ilhali yanakubalika mbele za Mungu katika Yesu Kristo, yanastahili kuhesabiwa haki. Tunakanusha kwamba katika maisha haya mapambano yetu dhidi ya dhambi iishiyo ndani mwetu yatakoma, japokuwa dhambi haina tena utawala juu yetu.

21 Abarikiwe yule Mungu na Baba wa Bwana yetu Yesu Kristo, ambaye ametubariki katika Kristo kwa kila baraka ya kiroho katika maeneo ya kiroho, kama vile alivyotuchagua katika yeye kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu kwamba tuwe watakatifu mbele zake (Efe. 1:3-4). Tazama pia Yohana 17:17; Mdo. 20:32; Rum. 6:5-6, 14; 8:13; 1 Kor. 6:11; 2 Kor. 7:1; Gal. 5:24; Efe. 3:16-19; 4:23-24; Flp. 3:10; Kol. 1:10-11; 2 The. 2:13; Ebr. 12:14.

*Kipengele 22* Tunasadiki kwamba Yesu Kristo ndiye mptanishi pekee kati ya Mungu na watu wake. Tunasadiki kazi ya Yesu Kristo kama Nabii, Kuhani, na Mfalme katika hali yake ya kufedheheshwa pamoja na hali yake ya kuinuliwa. Tunasadiki kwamba alitiwa mafuta na Roho Mtakatifu ili kwamba akatekeleze kazi ya huduma hii ya kipatanishi aliyoitiwa na Baba[22].

Tunakanusha kwamba Mungu amewahi kuwa, wala atawahi tena kuwa na kufanyika mwili kwingine au kwamba kumekuwa wala kutakuja kuwa na wapatanishi wa ukombozi mbali na Bwana Yesu Kristo. Tunakanusha wokovu mbali na Yesu Kristo pekee.

*Kipengele 23* Tunasadiki kwamba akiwa Nabii mkuu wa Mungu, Yesu Kristo alikuwa ndiye maudhui na lengo la unabii. Tunathibitisha kwamba Yesu Kristo alifunua na kutangaza mapenzi ya Mungu, alitoa unabii kuhusu matukio ya wakati ujao, na yeye mwenyewe ndiye utimizo wa ahadi za Mungu[23].

Tunakanusha, kwamba Yesu Kristo aliwahi kutamka unabii wa uongo au neno la uongo, au kwamba alishindwa ama atakuja kushindwa kutimiza unabii wote unaomhusu yeye mwenyewe.

---

22 Kwa maana kuna Mungu mmoja na mpatanishi mmoja kati ya Mungu na wanadamu, yule mwanadamu Yesu Kristo (1 Tim. 2:5). Tazama pia Ayubu 33:23-28; Luka 1:33; Yohana 1:1-14; 14:6; Mdo. 3:22; Kol. 1:15; Ebr. 1:1-4; 5:5-6; 9:15; 12:24.

23 Na sasa ndugu zangu, najua kwamba mlitenda kwa kutojua, kama walivyofanya pia watawala wenu. Ila kile ambacho Mungu alikitabiri kwa vinywa vya manabii wote, kwamba Kristo wake angeteseka, amekwisha kutimiza. Hivyo basi tubuni, mrejee, ili dhambi zenu zifutwe, ili nyakati za kuburudisha zije kutoka uwepo wa Bwana, na kwamba amtume yule Kristo aliyeteuliwa kwa ajili yenu, Yesu, ambaye mbingu lazima zimpokee hadi ule wakati wa kuvirejesha vitu vyote ambao Mungu aliuzungumzia zamani kwa vinywa vya manabii wake watakatifu. Musa alisema, ”Bwana atawainulia ninyi nabii kama mimi katika ndugu zenu. Mtamsikiza katika kila jambo atakalowaambia” (Mdo. 3:17-22). Tazama pia Mt. 20:17; 24:3; 26:31, 34, 64; Marko 1:14-15; Luka 4:18-19, 21; Yohana 13:36; 21:22; 1 Kor. 1:20; Ebr. 1:2; Ufu. 19:10.

*Kipengele 24* Tunasadiki kwamba Yesu Kristo ndiye Kuhani Mkuu wetu kwa mfano wa Melkizedeki, akiwa amekwisha kutoa dhabihu kamilifu ya yeye mwenyewe kwa niaba yetu na akiendelea kutuombea mbele za Baba. Tunasadiki kwamba Yesu Kristo ndiye mhusika na ndiye lengo la dhabihu kuu ya upatanisho[24].

Tunakanusha, kwamba Yesu Kristo, akiwa ametoka katika kabila la Yuda na sio kutoka kabila la Lawi, hakustahili kuwa kuhani wetu. Tunakanusha, kwamba anaendelea kujitoa kila wakati kama dhabihu katika Misa akiwa kafara na kuhani, hata kwa njia isiyo na damu. Tunakanusha kwamba alifanyika kuhani mbinguni pekee na kwamba hakuwa kuhani duniani.

*Kipengele 25* Tunasadiki kwamba kama Mfalme, Yesu Kristo anatawala kwa ukuu juu ya mamlaka yote ya duniani na yasiyo ya duniani sasa na hata milele[25].

Tunakanusha kwamba ufalme wa Yesu Kristo ni ufalme wa kisiasa tu wa ulimwengu huu. Tunakanusha kwamba watawala wa duniani hawawajibiki kwake.

---

24 Kwa maana Kristo ameingia, sio katika mahali patakatifu palipotengenezwa kwa mikono, ambako ni nakala ya pale pa kweli, ila mbinguni kwenyewe, sasa kusimama mbele za Mungu kwa niaba yetu. Wala haikuwa kwa ajili ya kujitoa yeye mwenyewe mara nyingi, kama kuhani mkuu aingiavyo mahali patakatifu kila mwaka akiwa na damu ambayo sio yake, kwa sababu ingelimpasa kuteseka mara nyingi tangu kuwekwa kwa misingi ya ulimwengu. Lakini kama jinsi ilivyo, ametokea mara moja mwishoni mwa dahari ili kuiondoa dhambi kwa ile dhabihu ya yeye mwenyewe. Na kama tu ilivyoamriwa kwa mwanadamu kufa mara moja na baada ya hapo huja hukumu, ndivyo pia Kristo akisha kutolewa mara moja ili kuzichukua dhambi za wengi, atatokea mara ya pili, sio kushughulikia dhambi bali kuwaokoa wale wanaomsubiri kwa shauku (Ebr. 9:24-28). Tazama pia Yohana 1:36; 19:28-30; Mdo. 8:32; 1 Kor. 5:7; Ebr. 2:17-18; 4:14-16; 7:25; 10:12, 26; 1 Pet. 1:19; Ufu. 5:6, 8, 12-13; 6:1, 16; 7:9-10, 14, 17; 8:1:12:11; 13:8; 15:3.

25 Kwa maana lazima atawale mpaka atakapowaweka maadui zake wote chini ya miguu yake (1 Kor. 15:25). Tazama pia Zab. 110; Mt. 28:18-20; Luka 1:32; 2:11; Mdo. 2:25, 29, 34; 4:25; 13:22, 34, 36; 15:16; Rum. 1:3; 2 Tim. 2:8; Ebr. 4:7; Ufu. 3:7; 5:5; 22:16.

*Kipengele 26* Tunasadiki kwamba wakati Yesu Kristo atakapowashinda maadui wake wote, atautoa ufalme wake kwa Baba. Tunasadiki kwamba katika mbingu mpya na nchi mpya, Mungu atakuwa pamoja na watu wake, na kwamba waumini watamwona Yesu Kristo ana kwa ana, watafanywa kuwa kama yeye, na watamfurahia milele[26].

Tunakanusha kwamba lipo tumaini lolote lile kwa wanadamu au jina lolote au njia ambapo wokovu unaweza kupatikana isipokuwa katika Yesu Kristo pekee.

---

26 Kisha unakuja mwisho, anapoutoa ufalme kwa Mungu Baba baada ya kuangamiza kila utawala na kila mamlaka na nguvu. Kwa maana lazima atawale mpaka atakapowaweka maadui zake wote chini ya miguu yake. Adui wa mwisho kuangamizwa ni mauti. Kwa sababu "Mungu amevitiisha vitu vyote chini ya miguu yake." Lakini inaposema "amevitiisha vitu vyote" ni wazi kwamba hajajumuishwa yeye aliyevitiisha vitu vyote chini yake. Wakati vitu vyote vitatiishwa kwake, basi Mwana mwenyewe pia atatiishwa kwake yeye aliyevitiisha vitu vyote chini yake ili kwamba Mungu awe vyote katika wote (1 Kor. 15:24-28). Tazama pia Isa. 65:17; 66:22; Flp. 2:9-11; 2 Pet. 3:13; 1 Yohana 3:2-3; Ufu. 21:1-5; 22:1-5.

# Insha Fafanuzi

*Fafanuzi*
*pamoja na*
*Mapendekezo kwa ajili ya*
*matumizi*

Siku moja dunia nzima italia kwa ungamo moja pekee: ”Yesu Kristo ni Bwana” (Flp. 2:11). Sentensi hii fupi imejawa na maana. Kusema kwamba Yesu ndiye Kristo ni kusema kwamba yeye ndiye “Mpakwa Mafuta.” Ni kusema kwamba yeye ndiye Masihi aliyeahidiwa na kusubiriwa kwa muda mrefu.

Kusema kwamba Yesu Kristo ni Bwana ni kusema kwamba yeye ni Mungu kweli wa yule Mungu kweli. Kufanyika mwili ni jambo la ajabu, siri inayoduwaza. Mungu alifanyika mwili. Hata kumwita Yesu ni kusema kwamba yeye ndiye yule mwokozi wa pekee. Alikuja katika ulimwengu huu akiwa na misheni ya kuwaokoa watu wake kutoka kwenye dhambi zao (Mt. 1:21).

“Yesu Kristo ni Bwana” ni kauli ya imani—tamko hakika la imani. Neno la Kiingereza creed linatokana na neno la Kilatini credo, ambalo linamaanisha “naamini.” Kanuni hii fupi ya imani inatangaza kile tunachokiamini kumhusu Kristo. Wengine hudhani kwamba 1 Tim. 3:16 inaweza pia kuwa tamko la kanuni ya imani. Sababu mbili huelekeza kwenye wazo hili. Kwanza, Paulo anautumia msemo huu, “Ni kuu, kweli, tunaungama. Pili, virai vya mstari huu ni vyenye mahadhi na vilivoelezwa kishairi. Virai hivi vinatengeneza muhtasari sahihi wa Kristo aliyefanyika mwili:

> Alidhihirishwa katika mwili,
> Akathibitishwa na Roho,
> Akaonekana na malaika,
> Akahubiriwa miongoni mwa mataifa,
> Akaaminiwa katika ulimwengu,
> Akachukuliwa juu katika utukufu (1 Tim. 3:16)

Mtindo wa kibiblia ni muhimu. Wakati kanisa la pale mwanzo lilifanya mitaguso na kuzalisha matamko ya imani, hawakuwa wakibuni mbinu mpya ya kuungama imani. Walikuwa wakiendeleza desturi iliyothibitika katika Maandiko.

Changamoto zilipoibuka, kanisa la pale mwanzo lilichukua msimamo. Isitoshe, wengi hufikiri kwamba mahitaji ya kiluturujia, au hamu ya ibada safi, ililichochea kanisa kujishughulisha na kuziandika hizi kanuni za imani. Hii ni kweli hususan kuhusu fundisho la Kristo. Ukweli wa kimsingi wa nafsi na kazi ya Yesu Kristo umekuwa ndio alama ya kutofautisha ya

Ukristo katika karne zote zilizopita.

Waandishi wa Agano Jipya wenyewe walipambana na dhana za uongo kuhusu utambulisho wa Kristo na kazi yake. Katika karne za pale mwanzo za kanisa, vikundi mbali mbali vilipinga uanadamu wa kweli wa Kristo. Kikundi kimoja, Wadoketi, walidai kwamba Yesu "alionekana" tu kuwa mwanadamu Uzushi mwingine, kama vile Uariani, ulipinga uungu wa kweli wa Kristo. Uzushi huu ulidai kwamba Kristo alikuwa hajamfikia Mungu Baba. Vikundi vya baadaye vilifanya makosa katika kueleza jinsi zile asili mbili, ule ubinadamu wa kweli na uungu wa kweli zimeungana katika nafsi moja. Kanisa la pale mwanzo lilijibu upinzani huu pamoja na makosa kwa kuita mitaguso na kuandika kauli za imani zilizotoa muhtasari wa mafundisho ya Biblia kuhusu zile kweli za kimsingi za imani ya Kikristo. Imani hizi ni urithi wenye thamani unaopitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Kwa hiyo leo tunazo rasilimali za Kauli ya Imani ya Mitume, Kauli ya Imani ya Nikea, na Fasili ya Kalsedonia. Kauli hizi za imani ni alama za mipaka, zikionyesha tofauti dhahiri kati ya usahihi na uzushi.

Kauli izi za imani zimetumika kulitia kanisa nguvu, na kwa mkono wa neema na wa utawala wa Mungu, zimewaongoza Wakristo katika kuitangaza Injili kwa uaminifu. Zinakaririwa leo hii kama ushuhuda wa thamani zao zidumuzo. Zinatukumbusha kwamba Kristo yupo katikati mwa theolojia yetu na pia katikati mwa ibada yetu. Kauli hizi za imani huliita kanisa "kuishindania imani iliyotolewa mara moja kwa watakatifu" (Yuda 1:3).

Lakini kauli hizi za imani hudokeza tu ile kazi ya Kristo. Hazifafanui kitimilifu Injili. Mgawanyiko wa kweli ulifanyika katika kanisa linaloonekana katika kipindi cha Marekebisho ya Kiprotestanti. Kazi ya Kristo ilikuwa ndio suala nyeti. Kimahususi zaidi, mjadala kuhusu fundisho la kuhesabiwa haki kwa imani pekee ulikuwa ndio ubishani mkuu uliochochea Marekebisho. Hapa, kanisa liligawanyika sehemu moja likiwa Uprotestanti na nyingine Ukatoliki wa Kirumi. Uprotestanti unasadiki fundisho la kuhesabiwa haki kwa imani pekee (sola fide), ilhali Ukatoliki wa Kirumi, ukifuata maagizo ya Mtaguso wa Trento unakataa fundisho la kuhesabiwa haki kwa imani pekee, ukichagua badala yake kuona kuhesabiwa haki kama kule kunakotokana na kushirikiana kwa imani na matendo. Marekebisho pia yalifichua tofauti katika suala jingine, ule ukuu na uongozi wa

kipekee wa Yesu Kristo juu ya kanisa lake na kwa kweli, juu ya vitu vyote.

Vikichukuliwa kwa pamoja, kauli za imani za kiekumeni za kanisa la pale mwanzo na mikazo hii ya Marekebisho vinatoa miongozo kwa kanisa kwa ajili ya kuhubiri Injili iliyo aminifu kibiblia. Kanuni za imani na yale maungamo mbali mbali ya Marekebisho na katekisimu hutoa mihtasari ya imani na huleta uwazi kwenye imani na Injili.

Neno Kafanyika Mwili: Tamko la Ligonier kuhusu Kristolojia kwa unyenyekevu linajaribu kulipa kanisa la kizazi hiki—na kwa baraka ya Mungu, vizazi vinavyokuja—tamko sahihi kuhusu nafsi na kazi ya Kristo linalochukua kutoka utajiri wa nyakati zilizopita, kutoka kwenye zile kanuni za imani za kiekumeni pamoja na theolojia ya Marekebisho. Pengine tamko hili pamoja na vipengele vyake 26 vinavyoambatana nalo vya kusadiki na kukanusha vinaweza kutumika kama kichocheo cha midahalo zaidi na kutafakari juu ya masuala haya muhimu ya Kristolojia. Pengine tamko hili lenyewe linaweza kuwa la manufaa hata kwa kanisa. Kila jitihada imefanywa ili kulifanya tamko hili liweze kuwa rahisi kukaririwa hadharani. Tunataka kila mtu anayekutana na tamko hili kujua kwamba "Yesu Kristo ni Bwana."

## TAMKO

Tamko hili lina beti au sehemu sita. Sehemu ya kwanza inatumika kama dibaji, ikiwa na vitenzi viwili muhimu: tunaungama na tunafurahia. Mungu amejifunua yeye mwenyewe pamoja na mapenzi yake katika kurasa za Maandiko. Ila bado yapo mambo ya siri ambayo ni ya kwake tu (Kum. 29:29). Lazima daima tuwe waangalifu kuhusu mapungufu yetu katika kazi ya theolojia. Kwa hiyo tunaanza kwa kuungama siri na maajabu ya Injili. Zingatio la msingi la tamko hili ni kule kufanyika mwili, ambako tunakupambanua kwa kifupi kama Mungu kafanyika mwili. Nafsi ya Kristo mara moja inapeleka kwenye kazi ya Kristo, kwa hiyo tunafurahia kwa pamoja kazi ya Kristo ya wokovu.

Ubeti wa pili unatilia mkazo uungu wa kweli wa Kristo, ukimwona akiwa katika nafasi ya usawa miongoni mwa zile nafsi tatu katika Uungu wa Utatu. Ubeti huu unahitimishwa kwa kutamkwa tena kwa ile fomyula ya Kikalsedonia kutoka kwenye Fasili ya Kalsedonia. Tangu kufanyika mwili Kristo amekuwa, na daima atakuwa asili mbili katika nafsi moja.

Ufafanuzi wa kufanyika mwili unachukua ubeti wa tatu ukitilia mkazo

ubinadamu wa kweli wa Kristo. Alizaliwa. Yeye ni Imanueli linalomaanisha “Mungu pamoja nasi” (Mt. 1:23). Hapa tunaungama kifo chake, kuzikwa, ufufuo, kupaa, na ujio wa pili. Hizi ndizo kweli za kihistoria za kufanyika mwili.

Kweli za kitheolojia za kufanyika mwili zinafuata katika sehemu ya nne, zikichukua kutoka umaizi uliopatikana tena kutoka wakati wa Marekebisho. Kwa niaba yetu, Yesu alikuwa mtiifu kamili. Yeye aliiweka sheria (utii wa kutenda) na akapokea adhabu ya sheria (utii wa kutendewa). Alikuwa mwanakondoo asiye dosari, akifanya upatanisho mbadala kwa ajili yetu. Alitatua tatizo lenye shinikizo kuu kuliko yote linalowakumba wanadamu: ghadhabu ya Mungu mtakatifu. Ubeti huu unahitimishwa kwa kutangazwa kwa fundisho la kuhesabiwa. Dhambi zetu zilihesabiwa kwake Kristo, ilhali haki yake ilihesabiwa kwetu sisi. Tunayo amani na Mungu kwa sababu moja tu na ya kipekee, kwa sababu ya kile ambacho Kristo alikifanya kwa ajili yetu. Tumevikwa haki yake.

Kile cheo chenye sehemu tatu (munus triplex) cha Kristo ni muundo wenye manufaa wa kitheolojia unaoeleza kwa usahihi kazi ya Kristo. Vile vyeo vitatu vya nabii, kuhani, na mfalme vilikuwa majukumu tofauti ya kipatanishi katika Agano la Kale. Yesu anayachanganya majukumu yote matatu katika nafsi yake moja, na anayatekeleza yote kikamilifu. Hapa tunatafakari sio tu kazi ya kipatanishi ya Kristo msalabani katika wakati uliopita, bali pia kazi yake sasa kama anaetuombea akiwa mkononi wa kuume wa Baba.

Ubeti wa kuhitimisha unathibitisha lile ungamo moja sahihi: Yesu Kristo ni Bwana. Theolojia yote ya kweli huongoza hadi kwa kuabudu Kwa sababu hiyo, tamko linahitimishwa kwa kitenzi muhimu tunalisifu. Kwa kumwabudu Kristo sasa, tunajiandaa kwa ajili ya kazi yetu ya milele.

### VIPENGELE ISHIRINI NA SITA VYA KUTHIBITISHA NA KUKANUSHA

Virai vya tamko hili ni malango ya kuingia katika somo la Kristolojia, vikivutia kwenye upelelezi wa thamani kuu ya mafundisho ya kibiblia kuhusu nafsi na kazi ya Kristo. Ili kutuongoza zaidi, vipengele ishirini na sita vya kuthibitisha na kukanusha vimeongezwa, kila moja kikiwa na ithibati zinazoandamana navyo za kimaandiko. Andiko moja kuu limeandikwa kitimilifu kwa kila moja ya vipengele, maandiko mengine

ya kuunga mkono pia yakitolewa. Vipengele hivi ni muhimu. Vinaweka mipaka ya mafundisho ya kibiblia kuhusu nafsi na kazi ya Kristo.

Kipengele 1 kinatumika kama dibaji, kikithibitisha kule kufanyika mwili.

Kipengele 2 kinatangaza uungu wa kweli wa Kristo, ilhali vipengele 2-5 vinaweka wazi ile Kristolojia ya Biblia ya nafsi moja, asili mbili. Vipengele 6-9 vinafunua ubinadamu wa kweli wa Kristo. Vipengele 10-26 vinageuka kutoka kwenye nafsi ya Kristo na kwenda kwenye kazi ya Kristo. Hivi vinaanza kwa kuthibitisha kazi ya wokovu na kuhitimishwa kwa maelezo ya kile cheo chenye sehemu tatu cha Kristo.

Makanusho yana umuhimu mkuu. Ni kinyume na mtindo katika enzi zetu za kustahimiliana kukanusha imani fulani, lakini vipengele hivi vya kuthibitisha na kukanusha sio tu zoezi la kujidhania lenye kiburi. Badala yake, vinatolewa kwa matumaini ya kulisaidia kanisa kusalia katika eneo salama na lenye lishe la mafundisho ya kibiblia. Yohana wa Pili 9 husema, "Yeyote anayeendelea wala asidumu katika mafundisho ya Kristo, hana Mungu." Hii Inaashiria kwenda zaidi ya mafundisho ya kibiblia kumhusu Kristo, au kwenda nje ya mipaka iliyoagizwa ya Kristolojia kama ilivyofunuliwa katika Neno la Mungu. Kadiri vipengele vile ishirini na sita vinavyopambanua ile mistari mbali mbali ya tamko, ndivyo vipengele vyenyewe vinavyoweza kupeleka kwenye mafundisho ya kina kirefu zaidi kumhusu Kristo.

Wengine wanaweza kuuliza kwa usahihi kwa nini tamko jipya linahitajika. Hilo ni swali zuri. Kwa sababu ya hilo tunatoa sababu tatu kwa ajili ya tamko hili. Tunaamini litatumikia ibada ya kanisa na mafundisho kwa wakati huu kwa kushughulikia changamoto za kale na za wakati uliopo. Tunaamini pia kwamba litawapa wala wanaohudumu katika Injili namna ya kuwatambua wengine ambao kweli ni wahudumu wenza. Hatimaye, tunahisi kwamba nyakati za changamoto kwa kanisa zipo upeoni wa macho, na tunaamini kwamba tamko hili litatukumbusha sote ile dhati ya Injili — uzuri wake, kuhitajika kwake, na udharura wake. Zingatia kila moja ya sababu hizi:

### KWA AJILI YA IBADA NA KUJENGEKA

Ligonier kwa unyenyekevu inatoa tamko hili kwa kanisa. Kuanzia karne za pale mwanzo, Wakristo wametumia kanuni za imani katika liturujia ya kanisa. Tunatumai kwamba tamko hili litaweza kutumika kwa lengo

lilo hilo. Kauli za imani zinaweza kuwa vifaa vyenye manufaa vya kufunza ili kupeleleza nyanda pana za mafunzo ya kibiblia. Tunatumai pia kwamba tamko hili na vile vipengele ishirini na sita vinaweza kutumika katika kanisa kama mwongozo wa upelelezi zaidi wa kibiblia na tafakari. Mafundisho ya nafsi na kazi ya Kristo ni muhimu kwa utambulisho na afya ya kanisa. Kila kizazi cha kanisa kinahitaji kuufunza na kuuthibitisha upya ule ufahamu sahihi wa nafsi na kazi ya Kristo. Tunaamini tamko hili litakuwa la msaada.

### LENGO LETU SOTE NI INJILI

Kuna idadi inayoongezeka ya makanisa yasiyo dhehebu, au mashirika, na harakati ulimwenguni—nyingi zikitumika kuisogeza Injili mbele. Mara nyingine inaweza kuwa vigumu kutambua ni wapi ambapo patakuwa na ushirikiano thabiti. Pengine tamko hili linaweza kutumika kuwatambua ndugu na dada katika Kristo na kuleta pamoja kazi mbali mbali kwa ajili ya Injili.

### KWA WAKATI KAMA HUU

Katika mji wa chuo kikuu wa Oxford umesimama Mnara wa Wafiadini, ukiwa ni ukumbusho wa kujitoa walikojitoa baadhi ya Warekebishaji Waingereza wa Marekebisho ya Kiprotestanti kama vile Thomas Cranmer, Nicholas Ridley, na Hugh Latimer. Unasema kuwahusu kwamba walitoa miili yao iteketezwe, wakishuhudia zile kweli takatifu walizothibitisha na kudumisha dhidi ya makosa ya Kanisa la Roma, wakifurahia kwamba walikuwa wamepewa sio tu kumwamini Yesu Kristo, bali pia kuteseka kwa ajili yake.

Waliamini, walithibitisha, na walizidumisha zile kweli takatifu za Injli ya Yesu Kristo. Katika kuzishuhudia kweli hizi, walizihubiri, walizitetea, na hata kuteseka kwa ajili yazo. Wengi katika karne zilizopita wamejiunga na Warekebishiaji hawa. Sehemu kubwa ya kanisa katika ulimwengu wa kisasa wa Magharibi imefurahia uhuru wa kidini. Ni kwa muda gani hali hii itaendelea kudumu huenda kukawa na shaka. Kizazi hiki au vizazi vinavyokuja huenda vikawa havina budi kuteseka kwa sababu ya kumwamini Kristo. Itakuwa sio hekima kabisa kuwa bila maandalizi, na pia sio hekima kukiacha kizazi kinachofuata bila maandalizi.

Hakika, kweli hizi kuhusu nafsi na kazi ya Kristo zinastahili kuaminika,

kuthibitishwa, kudumishwa, na kuteseka kwa ajili ya hizo.

Kulikuweko wakati katika maisha ya duniani ya Kristo ambapo umati wote ulikuwa umemuacha na akabaki na kundi lake la wanafunzi. Akawauliza kama wao pia wangemwacha. Petro akajibu kwa niaba ya kundi: "Bwana, tutaenda kwa nani? Wewe unayo maneno ya uzima wa milele, na tena tumeamini, na tumekuja kufahamu, kwamba wewe ndiwe yule Mtakatifu wa Mungu" (Yohana 6:68-69). Wakati mwengine baadaye, mmoja wa wale Kumi na Wawili akawa na mashaka yake, Yesu alikuwa ameshasulubiwa na kuzikwa. Kulikuweko ushuhuda wa kufufuka kwake, ila Tomaso alitilia shaka. Kisha Yesu akamtokea Tomaso. Akayagusa majeraha ya Kristo, majeraha aliyoyastahimili kwa ajili ya dhambi zetu. Tomaso akaungama, "Bwana wangu na Mungu wangu!" (Yohana 20:28).

Ndivyo tunavyoamini. Ndivyo tunavyoungama.